



JARIDA LA
MASIKINI
NA MAZINGIRA

ISSN 0821-6528

HUTOLEWA MARA MBILI KWA MWAKA NA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

TOLEO LA 8

JAN-JUNI 2010

Shein aieleza Afrika: Msidharau maarifa ya asilia katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazolikabili bara la Afrika



JARIDA LA UMASIKINI NA MAZINGIRA



Picha ya Jalada: Makamu wa Rais akihutubia katika maadhimisho ya siku ya mazingira Afrika, 3 Machi, Arusha Tanzania.

Lengo la Jarida la Umaskini na Mazingira

Jarida hili linatolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR), Idara ya Mazingira kwa ufadhili wa Mradi wa Umaskini na Mazingira kwa lengo la kutoa elimu na kujenga uelewa wa jamii na wadau mbalimbali kuhusu uhusiano uliopo kati ya umaskini na mazingira. Taarifa na makala zilizochapishwa katika jarida hili, zitatoa elimu na maarifa kwa watu binafsi na jamii kwa ujumla, na hatimaye kuchangia katika usimamizi endelevu wa mazingira katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Yaliyomo:

- Shein aieleza Afrika: Msidharau maarifa ya asilia katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazolikabili bara la Afrika 3
- Tanzania Yaaswa kuendeleza uwekezaji kwa kuzingatia maendeleo endelevu 4
- Nukuu kutoka ziara ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Mkoani Ruvuma 5
- Majanga yanavyochangia kuongeza umaskini: maporomoko ya ardhi pamoja na mafuriko ya Same na Kilosa na madhara yake katika mazingira, kijamii na kiuchumi 6
- Yaliyojiri katika mkutano wa Copenhagen 10
- Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais astaafu 14

Bodi ya Uhariri

Mwenyekiti

Richard Muyugi

Wajumbe

Bonaventura Baya

Angelina Madete

Anna Maembe

Blandina Cheche

Mshauri

Siglinda Chipungaupi

Usanifu na Uchapaji

Penplus Ltd.

022 2182059

Shein aieleza Afrika: Msidharau maarifa ya asilia katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazolikabili bara la Afrika

Na: Said Ameir

Nchi za Afrika zimetakiwa kuimarisha maarifa asilia waliyonayo watu wake katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazolikabili bara hilo ikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi.

Makamu wa Rais Dk Ali Mohamed Shein akifunguamaadhimishoyasiku ya Mazingira ya Afrika yaliyofanyika mjini Arusha mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka huu mbali ya kutoa wito huo alisisitiza umuhimu wa matumizi ya maarifa hayo katika kulinda na kuhifadhi bionuai ambayo aliifaninisha na 'bima ya maisha' kwa uhai wa binadamu.

Aliwaeleza washiriki wapatao 300 kutoka barani Afrika na kwingineko duniani kuwa watu wengi barani Afrika ikiwemo Tanzania wanategemea rasilimali za mazingira katika shughuli zao za kujipatia kipato, kukidhi mahitaji yao ya msingi, vifaa vya ujenzi, nishati na matibabu.

Alibainisha kuwa "utajiri wa rasilimali hizo za mazingira yaani misitu, maji baridi, bahari na rasilimali nyingine ndio mhimili wa uhai wa binadamu" na kuongeza kuwa kwa kuzingatia ukweli kuwa asilimia 45 ya miti nchini Tanzania inatumika kwa tiba asilia ni uthibitisho zaidi kuwa ustawi wa binadamu unategemea mazao na huduma toka bionuai hivo.

Dk Shein aliweka wazi kuwa uthabiti

wa maarifa asilia hayatokani tu na uchunguzi sahihi tu bali ni matokeo ya kujifunza kutoka vizazi hadi vizazi.

Kwa hiyo alibainisha Makamu wa Rais kuwa "kutokana na utegemezi huo wa maarifa asilia mfumo huo badala yake umekuwa ukihifadhi na kulinda bionuai hiyo kinyume na mfumo wa kisasa ambao huiathiri"

Alitoa mfano wa matumizi ya kalenda asilia ya kuratibu shughuli za kilimo kwa kutumia mwenendo wa mwezi ukihusishwa na misimu ya mvua na baadhi ya jamii kutumia majira hayo kwa kutumia viashiria vya hali ya hewa kulingana na tabia ya mimea kijiografia asili

Dk Shein aliwaeleza washiriki wa mkutano huo kuwa bionuai ya Afrika imo hatarini kutokana na tishio la mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa

viumbe hivi sasa vinahangaika kujizoeza na mabadiliko hayo. Kufuatia hali hiyo Dk Shein alionya kuwa "watu wengi wanaweza kuathirika zaidi katika mifumo yao ya kuishi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa na shinikizo nyingine".

Makamu wa Rais alieleza kuwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni moja ya changamoto ya wakati huu kwa kuwa tabianchi, bionuai na ustawi wa binadamu vina uhusiano usioweza kutofautishwa.

"Kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanagusa moja kwa moja maisha yetu, chochote kitakachoathiri uwezo wa kuhimili wa kiekolojia wa moja ya rasilimali hizo kitaleta athari kwa wote" Dk Shein alimalizia.



Makamu wa Rais akihutubia katika maadhimisho ya siku ya mazingira Afrika, 3 Machi, Arusha Tanzania.

Tanzania Yaaswa kuendeleza uwekezaji kwa kuzingatia maendeleo endelevu

Na: Mwandishi wetu

Makamu wa Rais Dk Ali Mohamed Shein amebainisha kuwa kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania uvutiaji wawekezaji na majadiliano na makampuni makubwa ya uwekezaji kama ya madini ni changamoto kubwa katika kuendeleza, kutumia na kuhifadhi rasilimali za mazingira.

Akifungua Kikao cha Tisa cha Kamati ya Utekelezaji ya Shirika la Kimataifa la Taasisi ya Juu ya Ukaguzi wa Mazingira (INTOSAI) kilichofanyika mjini Dar es salaam mwezi Februari 2010 Dk Shein alieleza umuhimu wa kutayarisha mipango madhubuti ya mazingira ambayo inayafanya makampuni hayo kuwajibika kwa jamii.

“Ushirikiano na makampuni ya kimataifa hususan inapokuwa katika kuvutia wawekezaji na mashauriano katika uwekezaji mkubwa kama wa sekta ya madini inahitajika kuweka mazingira bora ya mipango ya mazingira ambayo inajumuisha makampuni hayo makubwa kuwajibika kwa jamii,” alieleza

Sambamba na hilo Makamu wa Rais aliwaeleza washiriki wa kikao hicho kutoka nchi za Argentina,

Brazil, Cameroon, Canada, China, Jamhuri ya Czech, Estonia, Fiji, Indonesia, Morocco, Norway, Poland, Afrika Kusini, Uingereza na wenyeji Tanzania kuwa serikali imekuwa ikiwekeza rasilimali nyingi ili kuhakikisha taifa linapata maendeleo endelevu.

“Sisi watanzania tunawekeza sehemu kubwa ya rasilimali zetu kuhakikisha kuwa shughuli zetu za maendeleo zinakuwa ni kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo” alieleza.

Dk Shein alibainisha kuwa wito wa kusimamia maendeleo endelevu kama jibu la changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi unahitaji nguvu za pamoja kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

“Wito wa kuzingatia maendeleo endelevu, kama suluhisho, kwa hakika unalazimu jitihada za pamoja zikihusisha serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, viwanda, wataalamu kama washiriki wa kikao hiki na wananchi,” alisisitiza

Dk Shein aliwaeleza washiriki hao kuwa katika mazingira ya sasa ambapo ulimwengu unategemeana na kuwa karibu, halikadhalika matatizo ya mazingira nayo yanavuka mipaka na kuenea

duniani kote.

Katika mnasaba huo alitaka serikali “kuhakikisha zinafanya jitihada za kuhakikisha masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanapewa kipaumbele na kushughulikiwa ipasavyo”

Kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabiliana na changamoto za mazingira nchini, Dk Shein alitaja kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira-NEMC, Idara ya mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo pamoja na majukumu mengine inahakikisha uhifadhi endelevu wa maliasili za taifa.

Alitanabahisha kuwa wakati serikali imeamua kuipa nguvu sekta ya kilimo chini ya mpango wa *Kilimo Kwanza* lakini serikali pia inaelewa hatari ambazo zinaweza kutokea kwa rasilimali na mazingira na kwamba inachukua tahadhari.

“ili kupunguza athari, serikali inahimiza matumizi bora ya madawa ya kilimo yanayozingatia mazingira kwa njia ya kuwa na mipango na matumizi bora ya ardhi” alifafanua

Makamu wa Rais alisisitiza kuwa kwa vile changamoto za

mazingira ikiwemo ya mabadiliko ya tabianchi ni suala la dunia nzima Tanzania inashirikiana na wadau wengine katika ngazi hiyo na ndio maana imetia saina mikataba mbalimbali yenye lengo la kuhifadhi mazingira.

“Tanzania haifanyi kazi pekee katika kushughulikia changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Nchi yetu imetia saina mikataba mingi yenye maudhui ya kulinda na kuhifadhi mazingira,” alisema.

Aliitaja baadhi ya mikataba hiyo kuwa ni ule wa Basel unaohusu kudhibiti usafirishaji na utupaji wa madawa hatari, Mkataba wa Kimataifa wa kudhibiti Uvuvi wa Nyangumi, Mkataba wa Kimataifa wa Sheria ya Bahari na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kudhibiti Jangwa.

Kuhusu athari za mazingira nchini Makamu wa Rais aliwaeleza washiriki wa kikao hicho kuwa miongoni mwa athari hizo ni uharibifu wa ardhi ambao umeathiri tija katika uzalishaji na ubora wa maji, kuyeyuka kwa theluji ya mlima wa Kilimanjaro na Meru, kuongezeka kiwango cha joto, kulipuka kwa volcano ya mlima Oldonyo Lengai na mafuriko ya miaka ya hivi karibuni kuwa ni miongoni mwa athari hizo.

Nukuu kutoka ziara ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Mkoani Ruvuma

Na: Mwandishi wetu

1.0 Utunzaji wa mazingira

“mnapoeleza msilime kwenye vyanzo vya maji mkubali, na wala msichukie kwani mkikaidi mtaharibu vyanzo hivyo na kuathiri upatikanaji wa maji... Dunia nzima hivi sasa imetaharuki, kuna mabadiliko ya tabianchi; hali ya hewa na miongo imebadilika, mvua hazijui msimu tena. Tuyatunze mazingira yatutunze na Ruvuma iendelee kuwa kijana” ujumbe wa Dk Shein kwa wananchi wa Kijiji cha Matogoro, kata ya Matogoro katika Manispaa ya Songea katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Manispaa hiyo.

2.0 Mbegu bora na kupiga vita umasikini

“uamuzi wa kuzalisha mbegu bora ili kukidhi mahitaji ya mbegu kwa wakulima wetu

kupitia taasisi za umma ni uamuzi wa serikali. Kilimo hakiwi kilimo bila ya mbegu bora. Nasaha zangu kwenu wananchi zitumieni mbegu hizi na pia zingatieni maelekezo kutoka kwa wataalamu wa kilimo ili tuongeze tija katika uzalishaji hatimae kuutokomeza umasikini” kauli yake kwa wananchi wa Mlale wakati akizungumza na wananchi baada ya kukagua shamba la ekari 200 la mbegu chotara za mahindi UH 6303 (wilaya ya Songea).

3.0 Kushiriki na kuchangia shughuli za maendeleo kupia vita umasikini

“wewe usiyetaka kuchangia kaa kimya usiwe mstari wa mbele kuwabugudhi na kuwabeza wenzako wanaochangia shughuli za maendeleo. Tuchangie kwa mujibu wa uwezo wetu ‘mso hili ana lile’” ujumbe wa Dk Shein kwa wananchi wa Mbinga akiwakumbusha umuhimu wa kuchangia shughuli za maendeleo ikiwemo elimu.



“Uongozi ni kuonyesha njia”. Makamu wa Rais Dk Ali Mohamed Shein akikagua shamba la ekari 20 la mahindi mkoani Ruvuma.

Majanga yanavyochangia kuongeza umaskini: maporomoko ya ardhi pamoja na mafuriko ya Same na Kilosa na madhara yake katika mazingira, kijamii na kiuchumi

Na: A. Maembe na K. Mudiguza

Uhusiano baina ya umaskini na uharibifu wa mazingira umefafanuliwa katika makala na mikakati mingi ya kimataifa na kitaifa. Uharibifu wa mazingira husababisha umaskini kwani hupunguza upatikanaji wa maji safi, rutuba katika udongo, bidhaa na huduma nyingine muhimu kwa afya na maisha ya binadamu. Umaskini nao husababisha uharibifu wa mazingira kwani hudhoofisha juhudi na uwezo wa binadamu kusimamia na kutumia rasilmali kwa njia endelevu (Assey na wenzake 2007, katika Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Katika Tanzania)

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao ni mhimili wa sera ya maendeleo Tanzania, unatambua na umeainisha kwa mifano kuwa mazingira bora ni msingi mkuu wa maendeleo endelevu na kupunguza umaskini.

Kitu kingine kinachotia moyo juu ya kupambana na umaskini hapa nchini kwetu ni kuwa sasa hivi Watanzania wanaelewanakufahamu kwamba uchumi wa nchi na maisha ya watu maskini hutegemea sana usimamizi bora wa mazingira na kuzuia majanga. Uchunguzi uliyofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Masuala ya Jamii (ESRF)

mwaka 2003 umeonesha kwamba mambo makuu yanayosababisha umaskini ni uchumi duni, uharibifu wa mazingira na kukosekana kwa utawala bora (Assey na wenzake, 2007)

Katika kuuelezea umaskini, kuna vigezo au mambo ambayo huchangia kupunguza au kuongeza umaskini (pull and push factors). Majanga kama mafuriko, vimbunga, milipuko ya volkano na ukame ni baadhi ya mambo ambayo huchangia kuongeza umaskini kwani huleta njaa, uharibifu wa mali na makazi ya viumbe, vifo, maradhi na madhara mengine ambavyo kwa ujumla wake hurudisha nyuma juhudi za jamii husika kujiletea maendeleo. Kwa mfano mafuriko husababisha uharibifu wa makazi, mali kama mifugo, chakula, miundombinu kama barabara, shule, reli, vituo vya afya, vyoo na sehemu za kutupa taka. Aidha uharibifu huu huongeza maradhi kutokana na ukosefu wa maji safi na salama.

Kwa mwaka 2009, nchi yetu imeshuhudia majanga kadhaa kama ukame, maporomoko ya ardhi na mafuriko ambayo kwa kiasi kikubwa yanahusishwa na mabadiliko ya tabianchi (climate change) yanayotokana na shughuli za kibinadamu. Makala hii inaelezea na kutathmini madhara ya maporomoko ya ardhi na mafuriko yaliyotokea mwezi Novemba 2009

na katikati ya mwezi Januari 2010 wilayani Same katika Mkoa wa Kilimanjaro na mafuriko yaliyotokea wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro mwishoni mwa mwaka 2009.

Wilaya ya Kilosa ambayo ina ukubwa wa kilomita za mraba 14,245 ni moja kati ya wilaya tano za Mkoa wa Morogoro ambao unapakana na mikoa ya Tanga, Arusha, Iringa, Pwani, Lindi, Ruvuma na Dodoma. Kwa mwaka 2009, idadi ya watu katika wilaya ya Kilosa ilikadiriwa kuwa 580,306, kati ya hawa, wanawake ni 291,064 na wanaume ni 289,242.

Wilaya ya Kilosa ina misimu miwili ya mvua ambayo ni vuli na masika. Vuli huanza Oktoba hadi Disemba na masika huanzia Machi hadi Mei. Wastani wa mvua kwa mwaka ni mm 1200 katika uwanda wa chini/tambarare. Uwanda wa kati mvua hunyesha kwa wastani wa mm 950 na uwanda wa juu kwa wastani wa mm 1600.

Wilaya ya Kilosa ina mito ipatayo 36. Kati ya hiyo, mito sita ambayo ni Mkondoa, Mkundi, Lumuma, Zombo, Msowero na Mkata inatiririsha maji kwa mwaka mzima. Mito mingine iliyobaki inakuwa na maji msimu wa mvua. Mto Kinyasungwi ambao ni wa msimu hupokea maji kutoka katika vijito

vingi vinavyoanzia mikoa ya Manyara, Singida, Arusha na Dodoma. Pamoja na Kinyasungwi, mito Lumuma na Nyakatwanga (Mkoa wa Dodoma) humwaga maji katika Mto Mkondoa, ambao unapita uwanda wa chini wa maeneo ya Kilosa na ndiyo unaosemekana ulichangia sana kusababisha mafuriko yaliyotokea mwaka 2009 mwezi wa Disemba.

Mvua nyingi zilizonyesha mwezi Disemba mwaka 2009 katika maeneo ya Mkoa wa Dodoma zilisababisha kujaa kwa Mto Mkondoa na hatimaye kuleta mafuriko katika vijiji vya wilaya ya Kilosa. Kiasi cha mm 107 za mvua zilirekodiwa mkoa wa Dodoma kwa kipindi cha masaa 24 kabla ya mafuriko haya kutokea (TMA, Disemba 2009).

Mafuriko haya yalikuwa mabaya zaidi kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na kilimo cha milimani kisichozingatia njia bora za kilimo kutumia kontua na makinga maji, kilimo cha kuhama hama, uchimbaji mchanga ndani na kando kando ya mito kunakosababisha mito kubadili mikondo yake, ukataji wa miti kwa wingi (kusikoendana na upandaji wa mingine) kwa ajili ya mbao, kuni na mkaa hasa katika vyanzo vya mito pamoja na uchimbaji wa madini. Hali hii imefanya uharibifu wa udongo, misitu na mapori na hivyo mafuriko na maji mengi yalipotokea yalipita bila kizuizi na kusababisha madhara makubwa.

Jedwali Na 1: Baadhi ya Miundombinuya Maji iliyoathirika na Mafuriko Kilosa (Visima)

Kata	Visima Vifupi	Visima Virefu	Idadi ya watumiaji
Kasiki	9	3	3000
Mbumi	4	1	1500
Mkwatani	12	-	3000
Magomeni	30	-	7500
Mabwerekwerek	48	-	12000
Chanzuru	15	-	3750
Kimamba A and B	15	-	2000
Jumla	133	4	32750

Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (Februari 2010)

Licha ya mafuriko kusababisha uharibifu wa visima vya maji, miundombinu ya barabara na reli iliharibiwa. Jumla ya kilomita 207 ziliathirika kwa viwango mbambali katika Mji wa Kilosa na barabara zitokazo mjini Kilosa kwenda maeneo mengine ya Mkoa na sehemu nyingine nje na ndani ya Mkoa. Sehemu za Reli ya Kati kutoka Kilosa kwenda Morogoro na Dar es Salaam na Kilosa kwenda Dodoma ziliathirika ambapo jumla ya kilomita 2.60 zililusika katika maeneo mbalimbali ya reli hiyo. Huduma za reli zilisitishwa na kufanya usafiri kwa shughuli za kijamii na kiuchumi kuwa shida sana (kigezo kikubwa cha kuongezeka kwa umaskini). Aidha, nguzo



Madhara ya mafuriko katika moja ya mtaa wa Mji wa Kilosa yaliyotokea Disemba 2009.

100 za umeme ziliaribika na kusababisha wakazi wa mji wa Kilosa na vijiji kadhaa kukosa umeme na Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco) kukosa mapato.

Ukosefu wa maji safi na salama kutokana na miundo mbinu ya maji kuharibiwa na mafuriko ilikuwa adha kubwa kijamii, kiuchumi na kiafya. Magonjwa yanayohusishwa na maji na mazingira machafu kama kuhara, kipindu pindu na malaria yaliongezeka baada ya mafuriko na kufanya jamii na Serikali kutumia fedha na rasilimali nyingi kushughulikia tatizo la mafuriko.

Madhara mengine yaliyotokea Kilosa ni uharibifu katika miundo mbinu ya elimu. Baadhi ya majengo ya shule za msingi na sekondari yaliathirika. Katika Mji wa Kilosa shule za msingi za Mkondoa, Madaraka na Mkwatani zilizingirwa na maji, na baadhi ya majengo yamebomoka na kufanya shule hizo kufungwa. Tathmini imeonesha kwamba shule hizi zipo kwenye uwanda wa chini wa Mto Mkondoa unaofurika wakati wa mvua nyingi. Aidha wakazi wamepoteza mazao yao yaliyokuwa ghalani na mashambani na kusababisha hali ya akiba ya chakula kwa sasa na kwa mwaka ujao kuwa tete. Aidha wakazi wamepoteza mali zao nyingine kama mavazi na samani.

Jedwali Na 2: Athari za mafuriko Kilosa katika mashamba kwa Kata 2

No.	Kata	Kijiji	Aina ya zao liloathirika	Ukubwa wa sham-ba (ekari)	Maelezo
1.	Kimamba	Kimamba A	Mpunga Mahindi	205 105	Mashamba haya yalifunikwa na mchanga mwingi na tope. Mazao yote yaliharibiwa. Mashamba hayawezi kutumiwa tena
2.	Mambwerbwere	Mamoyo	Mahindi Migomba Mihogo Ufuta Pilipili	971 2 4 3 2	Mashamba haya yamejaa tope. Ili kuyafufua zitahitajika juhudi kubwa

Chanzo: Halmashauri ya Wilaya Kilosa (Februari 2010)

Mkoa wa Kilimanjaro hususan wilaya ya Same ni sehemu nyingine ya nchi hii iliyokumbwa na janga la maporomoko ya ardhi na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa zinazohusishwa na El Nino pamoja na madhara yatokanayo na mabadiliko ya hali hewa. Mvua hizo zilinyesha kati ya miezi ya Novemba na Disemba 2009 na Januari 2010 na kusababisha athari kubwa kwa wakazi wa maeneo husika kwani baadhi ya wakazi walipoteza maisha, mifugo ilikufa, makazi na mali za waathirika yalisombwa na maporomoko na maji ya mafuriko, miundombinu na huduma mbalimbali za

jamii ziliaribika, kuondolewa kwa uoto wa asili na uharibifu wa mazingira.

Wilaya ya Same ni kati ya wilaya 7 zinazounda Mkoa wa Kilimanjaro na upo umbali wa kilomita 105 Kusini Mashariki ya Mji wa Moshi ambao ni makao makuu ya mkoa na ina ukubwa wa eneo za mraba zipatazo kilomita 5186 na jumla ya watu wapatao 211738 (Sensa ya watu 2002).

Mnamo usiku wa kuamkia tarehe 10 Novemba 2009, kijiji cha Mamba Myamba kilichopo katika Tarafa ya Goha, wilayani Same kilikumbwa na maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa zilizokuwa zikiendelea kunyesha katika maeneo mengi ya ukanda wa Milima ya Pare Kusini ambapo kijiji hicho kimo ndani ya milima hiyo ya uwanda wenye mwinuko zaidi ya mita 1200 kutoka usawa wa bahari, mteremko mkali na kilimo cha milimani kisichozingatia hifadhi ya mazingira. Maporomoko hayo yalileta athari kubwa kwani watu takriban 25 wa jinsia na rika mbalimbali walipoteza maisha kwa kufukiwa na kifusi cha mawe na udongo uliosababishwa na janga hilo. Pamoja na kupotelewa na nguvu kazi ya Taifa hili makazi, mali, mimea shambani, mifugo mazingira na miundombinu mbalimbali iliharibika kwa kiwango cha kutisha na hivyo kurudisha nyuma juhudi za wananchi katika kujikwamua kiuchumi.

Aidha kijiji cha Kihurio kilichopo Kata ya Kihurio wilayani Same kilikumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa zilizonyesha kwa siku 2 (tarehe 9 na 10 Januari 2010). Katika mafuriko hayo familia za watu zipatazo 215 zilipoteza makazi yao na kwa siku kadhaa watoto 2800 wa shule za msingi 19 zilizopo katika kata hiyo walishindwa kwenda shule baada ya Mto Wanchi uliopo eneo hilo kufurika. Barabara kuu itokayo Arusha/Moshi hadi Dar es Salaam ilifugwa kwa muda na kusababisha adha kubwa katika sekta ya usafiri. Sababu kubwa iliyochangia mafuriko haya kama yale ya Kilosa ni uharibifu wa mazingira uliotokana na kilimo cha milimani, uchimbaji wa mawe na kokoto na kufanya milima hii kuwa dhaifu



Maporomoko ya ardhi kijiji cha Mamba Myamba wilayani Same.

na hivyo kuporomoka baada ya maji mengi ya mafuriko ya mwezi Novemba mwaka 2009.

Jambo moja linalofanya mafuriko ya Kilosa kuwa tofauti na yale yaliyotokea Same mkoani Kilimamjaro ni kwamba wakazi wa Kilosa walitahadharishwa mapema na kuondoka eneo la mafuriko na hivyo kupunguza madhara ya vifo ambapo mtu mmoja tu ndiyo aliyefariki.

Ukiangalia madhara ya mafuriko haya kwa maendeleo ya wakazi wa Kilosa na Same ni makubwa na kufanya juhudi za kupunguza umaskini kwa wakazi hawa kurudishwa nyuma sana. Kipato cha wakazi wa Same

na Kilosa kinachotokana na shughuli za kijamii na kiuchumi kama kilimo na biashara ndogo ndogo kimepungua sana. Aidha akiba yao ya chakula imeharibiwa, na uwezo wa kugharamia elimu, matibabu na huduma nyingine za familia zao umerudi nyuma kutokana na kutokuwa na njia za kujipatia kipato. Wengi wa waathirika wa mafuriko haya kwa sasa wanaishi kwa kutegemea misaada kutoka Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika mbalimbali ya Serikali na Binafsi, Wasamaria wema, Msalaba Mwekundu, jamaa na marafiki. Aidha Serikali inatumia fedha nyingi kurudisha miundombinu iliyoharibika na kutoa huduma kwa jamii katika maeneo haya.

Yaliyojiri katika mkutano wa Copenhagen

Na Penzi Nyamungumi

Wadau wa mazingira kutoka pande zote za dunia walikutana katika mji mkuu wa Denmark, Copenhagen kuanzia tarehe 7 hadi 19 Disemba, 2009 kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Bella center mjini Copenhagen ulijumuisha mkutano wa 15 kuhusu Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na mkutano wa tano wa nchi wanachama wa Mkataba wa Kyoto.

Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki wapatao 40,000 wakiwemo wanasayansi, wataalam wa mazingira, wawakilishi wa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali

(NGO's) yanayoshughulikia masuala ya mazingira pamoja na waandishi wa habari.

Aidha, viongozi wa nchi na serikali karibu 115 walihudhuria mkutano huo wa pamoja wa serikali uliofanyika kati ya tarehe 16-18 Disemba na kuufanya moja ya mkutano mkubwa kuhudhuriwa na viongozi wa dunia nje ya New York .

Viongozi hao walipata nafasi ya kutoa hotuba kuhusu matarajio ya nchi zao katika suala zima la kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Ujumbewa Tanzania ulioongozwa na Makamu wa Rais Dk. Ali Mohamed Shein ulijumuisha mawaziri wanaoshughulikia masuala ya mazingira kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkutano wa Copenhagen ulifikia kilele baada ya mchakato wa miaka miwili wa majadiliano ulioanzia Bali, Indonesia mwaka 2007 na baadaye majadiliano kuendelea Poznan, Poland mwaka 2008.

Mkutano huo ulilenga kufikia makubaliano ya kisheria ya mkataba mpya utakaohusisha nchi zote duniani utakaotekelezwa sambamba na mkataba wa Kyoto ambao utekelezaji wake awamu ya kwanza utakamilika mwaka 2012.

Mazungumzo katika mkutano huo yaligawanyika katika sehemu mbili. Kwanza , majadiliano kuhusu kukamilisha maandalizi ya makubaliano ya kisheria ya kutekeleza mkataba wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 1992 kwa kuhusisha nchi zote duniani kwa misingi ya usawa na uwajibikaji kulingana na mchango wa nchi husika katika tatizo hili.

Pili, majadiliano kuhusu kuhakikisha nchi zilizoendelea zinapunguza gesijoto kulingana na makubaliano ndani ya mkataba wa Kyoto baada ya mwaka 2012 ambapo awamu ya kwanza ya utekelezaji ya mkataba huo utakapokamilika.

Chini ya makubaliano mapya, matarajio ya Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazoendelea yalikuwa ni kuona nchi zilizoendelea zinakubali kupunguza uzalishaji wa gesijoto angalau kwa asilimia 40 chini ya viwango vilivyokuwa vikizalishwa mwaka 1990 ifikapo mwaka 2020.



Makamu wa Rais Mh. Dk. Ali Mohamed Shein akihutubia mkutano wa Kimataifa wa Tabia Nchi mjini COP 15 Copenhagen Desemba 2009.



Baadhi ya wadau wa mazingira kutoka pande zote za dunia walikutana katika mji mkuu wa Denmark, Copenhagen kuanzia tarehe 7 hadi 19 Disemba, 2009

Akizungumza na waandishi wa habari Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Dk. Batilda Burian alisema kuwa matarajio mengine kutoka katika mkutano huo yalikuwa ni kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea.

“Afrika kwa ujumla ilitaka ipate asilimia tano (5%) ya pato la taifa la nchi zilizoendelea (takriban dola bilioni 400 kwa mwaka) kuanzia mwaka 2012,” alisema waziri Batilda na kuongeza kuwa “nusu ya fedha hizo tulitaka zitumike katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika nchi za Afrika.”

Kwa mujibu wa Waziri Batilda Tanzania pia ilikuwa inatarajia katika

mkutano huo kuboresha utaratibu wa kushiriki katika miradi ya kupunguza gesijoto ili kuhakikisha nchi za Afrika zinafaidika na mfumo huo.

“Hii itaongeza fursa kwa makampuni binafsi ya Tanzania kushiriki katika miradi hii na kujenga uwezo wa kitaifa wa kushiriki katika miradi inayoweza kukuza uchumi bila kuharibu mazingira,” alibainisha Dk. Batilda.

Aidha Tanzania ilikuwa na matarajio ya kupata fursa, fedha na teknolojia kwa ajili ya kujenga uwezo wa nchi za Afrika katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha utaratibu wa matumizi ya misitu katika kunyonya gesijoto unazisaidia nchi zenye misitu kama Tanzania kupata maendeleo endelevu.

Hata hivyo, kulikuwa na mvutano kati ya nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea wakati wa majadiliano katika mkutano huo ambapo kila upande umekuwa ukivutia kwake. Hata hivyo, majadiliano hayakufikiwa kama ilivyotarajiwa.

Hali hiyo ilitagemewa kutokea kwa kuwa nchi zilizoendelea ambazo ndizo wahusika wakuu katika kuunguza dunia hii hawakuwa tayari kutangaza viwango vyao vya kupunguza gesijoto. Sababu kubwa ni kwamba kwa kufanya hivyo kwao ni kuathiri uchumi utokanao na uzalishaji viwandani.

Kwa upande mwingine nchi zinazoendelea zikiwemo za Bara la Afrika ambalo ndilo waathirika wakuu wa mabadiliko ya tabianchi zilikuwa zinataka mkutano huo

utoke na makubaliano ya kisheria ya kuzibana nchi zilizoendelea kutimiza wajibu wao. Makubaliano ya kisheria hayakuwezekana.

Kufuatia mvutano huo Waziri Mkuu wa Denmark Lars Lokke Rasmussen ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mkutano ngazi ya viongozi wa nchi aliitisha kikao cha marais 24 ambao walikaa na kuandaa waraka unaojulikana kama “Copenhagen Accord” ambao ulikosolewa na nchi nyingi zinazoendelea ikiwemo Afrika.

Hii inatokana na muafaka huo kutozingatia upunguzaji wa gesijoto duniani ili kutozidi nyuzijoto 1.5 ifikapo 2020 ambao ndio msimamo wa nchi za Afrika. Aidha, suala la fedha za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hatua zinazochukuliwa na kila nchi husika

ilionekana ni changamoto na nchi zilizoendelea zilikubali pawepo na makubaliano ya kiungwana badala ya makubaliano ya kisheria.

Baadhi ya nchi zililalamika kuhusu ukosefu wa uwazi katika suala zima la kuupata Waraka huo. Idadi ndogo ya nchi zinazoendelea, Venezuela, Bolivia, Cuba na Nicaragua zikiwa mstari wa mbele walipinga vikali na kuushutumua mchakato huo na kusemahaukupatikanakwa uwazi na wala sio kwa njia ya kidemokrasia.

Nchi nyingi zimekuwa zikipigania kufikiwa kwa makubaliano ya kisheria katika mkutano huo kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo tayari zimejitokeza katika baadhi ya nchi ikiwa ni pamoja na Tanzania.

“Nchi kama Tanzania imeathirika:

ukame na mafuriko ya mara kwa mara, ugonjwa kama malaria hivi sasa unapoteza maisha ya watu kwenye maeneo ambayo ugonjwa huo haukuwepo kabla, mito inakauka, kuongezeka kwa maji ya bahari kunaharibu miundombinu ya maeneo ya pwani na visiwa vidogo vinazama,” alisema Dk. Shein.

Kiongozi wa Maldives alielezea jinsi visiwa hivyo viko katika hatari ya kuzama na kusema hata Baraza la Mawaziri la Visiwa vya Maldives Oktoba, 2009 lilifanya kikao chake chini ya bahari. Huko Nepal barafu ya Mlima Everest, kama ilivyo kwa Mlima Kilimanjaro hapa nchini inakabiliwa na tishio la kuyeyuka kabisa.

Kufuatia hali hiyo, viongozi wa Afrika walisisitiza haja ya nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zake



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mh. Dk Batilda Burian akiwa kwenye mkutano wa Kimataifa wa Tabia Nchi COP 15 Copenhagen Desemba 2009.

za kupunguza gesijoto alau kwa asilimia 45 ya viwango vya mwaka 1990 ili kuifanya dunia kuwa mahala salama pa kuishi.

Walisitiza pia misaada ya kifedha na teknolojia itolewe kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Athari hizo ambazo zilitajwa na viongozi mbalimbali na hasa wa kutoka nchi zinazoendelea zilimfanya Waziri wa Mazingira wa Sweden, kwa niaba ya Jumuiya ya Ulaya kueleza umuhimu wa kufikia makubaliano ya kisheria katika mkutano huo ili kuifanya dunia kuwa mahala salama pa kuishi.

Kwa ujumla viongozi wote waliozungumza katika mkutano huo wanakubali kuwa mabadiliko ya tabianchi yameleta athari kubwa na hasa kwa nchi maskini na kwamba kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kukabiliana na tatizo hilo .

“Katikamkutano ule hakuna kiongozi aliyekataa kuwa mabadiliko ya tabianchi sio tatizo. Wote walikubali kuwa ni tatizo, baadhi yao walisema tuchukue hatua leo kabla ya kesho na wengine, tuchukue hatua sasa hivi,” alisema Dk. Shein alipozungumza na waandishi wa habari katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere mara baada ya kuwasili kutoka Copenhagen .

Rais Barack Obama wa Marekani alieleza wazi kuwa hakwenda Copenhagen kwa ajili ya kuzungumza bali kuchukua hatua zinazofaa

katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuwataka viongozi kufikia makubaliano ya kisheria.

Pamoja na mvutano huo, mkutano haukupitisha mapendekezo yaliyotolewa bali uliutambua muafaka wa Copenhagen na kuazimia kuufanya kama ni moja ya nyarakaza msingi katika kukamilisha majadiliano yatakayoweka mkataba wa kisheria katika kikao cha 16 cha nchi wanachama Mexico Disemba, mwaka 2010.

Hata hivyo, jambo ambalo wengi walionanika mafaanikiomakubwa kwa upande wa Waraka huo, yaani “Copenhagen Accord” linahusiana na misaada ya kifedha ya muda mfupi na mrefu. Nchi zilizoendelea zilikwenda Copenhagen zikiwa na ahadi za kusaidia miradi ya kupunguza gesijoto na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zinazoendelea.

Kwa mujibu wa Waraka wa Copenhagen nchi hizo zimekubali kutoa dola za Kimarekani bilioni 10 kwa mwaka kuanzia 2010-2012, kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea ambapo asilimia 40 ya fedha hizo zitakwenda kwa nchi za Afrika.

Kwa upande wa msaada wa kifedha wa muda mrefu nchi hizo zilisema ifikapo mwaka 2020 zitatoa dola za Kimarekani bilioni 100 kila mwaka kutoka kwenye vyanzo mbalimbali

kwa madhmunu hayo.

Hata hivyo, mkutano huo uliweka utaratibu chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Mataifa kwamba mataifa ambayo yanakubaliana na Waraka huo yajisajili na kupeleka viwango vyao vya kupunguza gesijoto ifikapo Januari 31, mwaka huu.

Mbali na waraka huo yaani “Copenhagen Accord” jambo jingine lililojitokeza na kuonekana ni mafanikio ya mkutano huo ni kwa Marekani kwa mara ya kwanza kutangaza azma yake ya kupunguza gesijoto kwa asilimia 17.

Sote tunatambua kuwa Marekani haijawahi kusaini Mkataba wa Kyoto na hivyo uamuzi wake huo ulipokewa na wajumbe wa mkutano huo kwa matumaini kwamba utaongeza nguvu katika mapambano ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa ujumla, mkutano wa Copenhagen unaonyesha bado kuna kazi kubwa ya kufanya kabla ya watu kuweza kuamini kwamba dunia imefungua ukurasa mpya katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Changamoto iliyopo hivi sasa ni kuyafanyia kazi masuala muhimu yaliyojadiliwa na kukubalika Copenhagen na kuyaweka katika makubaliano ya kisheria kwenye mkutano wa Mexico utakaofanyika Disemba mwaka huu.

Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais astaafu

Na: Mwandishi wetu

Bw. Eric K. Mugurusi, Mkurugenzi wa Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais amestaafu utumishi serikalini tarehe 24 Novemba 2009. Safari ya Bw. Mugurusi ya utumishi serikalini ilianzia kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, mnamo mwaka 1974, ambako alisimamia masuala ya Mipango Kamambe, Utafiti na Uratibu wa mazingira; wakati huo masuala ya mazingira hayakuwa yenye kipaumbele kama ilivyo sasa. Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira liliundwa baadae mwaka 1983 chini ya Wizara hiyo. Bw. Mugurusi aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idaraya Mazingira ilipoundwa kwa mara ya kwanza katika muundo wa Serikali, chini ya iliyokuwa Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira, mwaka 1990. Cheo hiki alikishikilia hadi alipostaafu mwaka jana. Baadaye, mwaka 1995, Idara ya Mazingira iliamishwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais; Bw. Mugurusi alihama nayo.

Uzoefu, ujuzi na mchango wa Bw. Mugurusi katika nyanja ya sera, mikakati, mipango na usimamizi wa mazingira unatambulika kwa wadau wa mazingira, kitaifa na kimataifa. Mchango wake unajidhihirisha wazi wazi katika Sera ya Taifa ya Mazingira, makala mbali mbali ya kisera, mikakati na mipango ya mazingira, ambayo yeye aliisimamia. Yeye ndiye aliyeratibu mchakato wa kitaifa wa maandalizi ya Mkutano wa

Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo, uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil mwaka 1992. Wakati wa mchakato huu, na kwa vipindi mbali mbali baadae, Bw. Mugurusi alitoa mchango wa kina katika majadiliano ya mikataba ya Kimataifa kuhusu mazingira, k.v. Mkataba kuhusu Bioanuai, Mabadiliko ya tabianchi, Kuenea kwa hali ya jangwa, Maendeleo endelevu ya ziwa Victoria, Maendeleo endelevu ya ziwa Tanganyika, na mingine mingi. Chini ya mikataba hii na mingine, programu na miradi mingi ilibuniwa na kutekelezwa chini ya Idara, na kupitia taasisi nyingine za umma na wadau mbali mbali. Hadi anastaafu Bw. Mugurusi alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kikanda ya usimamizi wa ziwa Tanganyika, kama chombo cha ushauri wa Mkutano wa Mawaziri wa nchi nne husika. Aidha, alikuwa katika timu ya kitaifa ya wataalam sita kwenye majadiliano ya nchi za kanda ya bonde la mto Nile.

Wakati wa utumishi wake, Bw. Mugurusi alikuwa mjumbe wa Bodi mbali mbali za kitaifa na za kimataifa, k.v. TANAPA, NEMC, TAZAMA, CPCT, nk. Kimataifa, alikuwa mwakilishi wa bara la Afrika kwenye Kamati Kuu ya nchi zilizoridhia mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi kutoka mwaka 2007 hadi 2009. Pia alikuwa mwakilishi pekee wa bara la Afrika kwenye Kamati ya Kimataifa ya ushauri kuhusu Uzalishaji na Matumizi endelevu ya rasilimali kutoka mwaka 2008 hadi alipostaafu.



Bw. Eric K. Mugurusi

Kwa hakika, ujuzi, uzoefu na msukumo wa Mkurugenzi Mugurusi ulikuwa mchango wenye mvuto katika changamoto za mazingira.

Baada ya kustaafu, Bw. Mugurusi alichaguliwa kuliwakilisha bara la Afrika kwenye Kamati ya Kimataifa ya wataalam kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi, wakati wa kikao cha 15 cha nchi zilizoridhia mkataba huu, huko Copenhagen, Denmark, mwezi Desemba 2009. Hivi majuzi, tarehe 29 Machi 2010, Kamati hii ilikutana mjini Bonn, Ujerumani na kumchagua Bw. Mugurusi kuwa Mwenyekiti.

Bw. Mugurusi ni mhitimu wa shahada ya Uhandisi kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, fani ya Upimaji na Ramani (1974); shahada ya pili ya Mipangomiji kutoka Chuo Kikuu cha Sydney, Australia (1978); aidha ni Humphrey Fellow wa Chuo Kikuu cha Massachusetts Institute of Technology (MIT), Marekani.